**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

**UMOJA WA SHULE ZA KIJESHI**

**MTIHANI WA KIDATO CHA NNE KABLA YA MTIHANI WA TAIFA**

**021** **KISWAHILI**

**MUDA: Masaa 3:00** **04 AGOSTI 2026**

---

MAELEKEZO

1 . Mtihani huu una sehemu tatu A , B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11) .

2 . Jibu maswali yote toka sehemu A na B ,na maswali mawili ( 02 ) toka sehemu C , swali la tisa ( 09 ) ni la lazima .

3 . Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kwa kila swali .

Shulelibrary.com

SEHEMU A ( Alama 16 )

1 . Chagua herufi ya jibu sahihi zaidi katika vipengele ( i ) hadi ( x ) kisha andika herufi ya jibu katika karatasi ya kujibia .

( i ) Chukulia kuwa unataka kujifunza jinsi ambavyo vitamkwa vya lugha ya Kiswahili vinavyoungana ili kujenga maneno yanayokubalika katika lugha ya Kiswahili . Je , ni utanzu gani wa sarufi utashughulika nao ili kupata uelewa wa mambo hayo ?

A . Fonolojia
B . Mofolojia
C . Sintaksia
D . Semantikia
E . Pragmatiki .

(ii ) Katika uchanganuzi wa sentensi , chagizo hutumika katika mkabala upi ?

A . Mkabala wa kimuundo
B . Mkabala wa kisiasa
C . mkabala wa kimapokeo
D . Mkabala wa kiupatanishi
E . Mkabala wa kisintaksia .

Shulelibrary.com

(iii) Neno “ cheza ” ni kitenzi kikuu na kitenzi kikuu huunda kishazi huru na kishazi tegemezi vilevile huundwa na kitenzi ila utofauti wake ni ………………

A . Kishazi tegemezi huundwa na vishazi vyenye viambishi vya o – rejeshi
B . Kishazi tegemezi huundwa na sehemu ya kiarifu inayokaliwa na kielezi
C . Kishazi tegemezi huundwa na vitenzi vyenye viambishi vilivyorejeshwa
D . Kishazi tegemezi huundwa na sehemu ya kiarifu inayokaliwa na nomino
E . Kishazi tegemezi ni mada ya sarufi tegemezi .

(iv) Hamsini , laki , enzi , sahil , kasri na fikiri ni miongoni mwa maneno yanayothibitisha asili ya Kiswahili kuwa ni :-

A . Kibantu
B . Kiingereza
C . Pijini
D . Kiarabu
E . Kijerumani .

(v ) Neno “ chawa ” lenye maana ya mfuasi au kibaraka wa mtu fulani linaweza

kuingizwa kwenye kundi gani la misimu ?

A . Misimu ya pekee
B . Misimu ya misimu
C . Misimu ya kitarafa
D . Msimu zagao
E . Misimu binafsi .

(vi ) Katika ufupisho wa habari yoyote ile inapaswa kuzingatia mambo yafuatayo isipokuwa …………………..

A . Kutumia maneno yako mwenyewe
B . Kubakiza maana ya habari ya awali
C . Kutumia herufi kubwa unapoandika
D . Kuwa na mtiririko mzuri
E . Kutokubadili majina ya mahali , watu au wanyama yaliyoainishwa katika habari ya awali .

(vii ) Katika lugha ya Kiswahili watu hufanya makosa mbalimbali pindi wanapozungumza . Je , katika sentensi " mfupa hauna ulimi " , mzungumzaji amefanya kosa gani katika lugha ?

A . Makosa ya kimatamshi
B . Makosa ya kimuundo
C . Makosa ya msamiati
D . Makosa ya kuacha neno
E . Makosa ya kimantiki .

Shulelibrary.com

(viii) Upatanisho wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili hutokea katika …………………

A . Nomino na kitenzi
B . Kitenzi na kivumishi
C . Kivumishi na kielezi
D . Kielezi na kiambishi
E . Kiambishi na sentensi .

(ix ) Miongoni mwa mambo yanayoipa uhai fasihi simulizi ni ushirikishwaji wa hadhira , unahisi ni jambo gani lingine linaweza kuipa uhai kazi ya fasihi simulizi .

A . Uibuaji wa hisia
B . Kutokuwa na gharama
C . Haibagui hadhira
D . Huhifadhiwa kichwani

E . Kuwa na tanzu chache .

( x ) Kirai ni neo au kikundi cha maneno mawili au zaidi ambacho huwa na sifa zifuatazo isipokuwa ……………….

A . Hutoa maana kamili
B . Huundwa na maneno mawili au zaidi
C . Huwa sehemu ya sentensi
D . Hakina kitenzi kikuu
E . Hakitoi taarifa kamili .

2 . Oanisha vipengele vya safu A na vile vya safu B ili kupata sentensi zenye upatanisho wa kisarufi .

| Safu A | Safu B |
|---|---|
| ( i ) Mtoto<br>(ii ) Walimu<br>(iii) Ukucha<br>(iv) Mazingira<br>(v ) Hospitali<br>(vi) Kiti | A . Umeanguka<br>B . Yamesafishwa<br>C . Amefaulu<br>D . Kimeletwa<br>E . Zimefungwa<br>F . Zimeokotwa<br>G . Vimeletwa<br>H . Wamesafiri<br>I . Vimeondolewa |

Majibu

| i | ii | iii | iv | v | vi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |

Shulelibrary.com

SEHEMU B ( Alama 54 )

Jibu maswali yote katika sehemu hii .

3 . ( a ) Andika nahau zenye maana sawa na tungo zifuatazo :-

( i ) Juma nne ni mchoyo
(ii ) Mwajuma ni mwizi
(iii) Ana amelewa sana

(iv) Mwalimu wetu ni mropokaji
(v ) Inatubidi tupige hatua na kuvumilia hadi tone la mwisho .

( b ) Watumiaji wengi wa lugha ya Kiswahili hufanya makosa katika utumiaji wa lugha aidha kwa kujua au kutokujua . Bainisha makosa manne ( 4 ) ya kisarufi yanayofanywa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kwa kutoa mifano dhahiri .

4 . Baada ya uhuru wa Tanganyika viliundwa vyama , asasi na taasisi mbalimbali za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili , japo zilijitokeza changamoto mbalimbali . Eleza changamoto sita (6 ) ambazo zilijitokeza kwa vyama , asasi na taasisi za ukuzaji Kiswahili .

5 . ( a ) Soma sentensi zifuatazo ambazo ni tata kisha eleza sababu za utata katika sentensi hizo .

( i ) Kicheko amepata jiko .
(ii ) Ana alimpikia baba chakula
(iii) Mama Musa amefika .
(iv) Baba alileta tai .

( b ) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia mkabala wa kimuundo kwa njia ya matawi . " Watu wote walimsikiliza Rais ."

Shulelibrary.com

6 . Suala la mmomonyoko wa maadili katika jamii linapaswa kuangaliwa kwa jicho la tatu ili kujenga jamii bora . Tumia tamthiliya ya Kilio Chetu kuonesha mambo sita ( 6 ) yaliyoibuliwa na mwandishi kama chanzo cha mmomonyoko wa maadili kwa jamii .

7 . Umechaguliwa kutoa risala kwa niaba ya wanafunzi wenzako katika siku ya mahafali yenu mbele ya Mgeni rasmi Waziri wa Elimu Tanzania , andaa risala itakayosomwa siku hiyo maalum ( zingatia muundo sahihi wa uandishi wa risala ) .

8 . Soma utanzu ufuatao kisha jibu maswali .

1 . Ninaanza kwa mtaja ,
Allah muumba **waja** ,
Mungu wetu mmoja ,
Katika hii dunia .

2 . Ninakuomba manani ,
Unipe yako **auni** ,

Nitoe yako moyoni ,
Wenzangu kuwausia .

3 . Yahusuyo mazingira ,
Katika yetu duara ,
Kuyalindeni kwa **dira** ,
Ndilo ninalowaambia .

4 . Zile fujo **mbadala** ,
Ndicho chanzo suala ,
Mazingira kitawala ,
Yawapo katika kutunzwa .

Maswali

( a ) Andika kichwa kinachofaa kwa utanzu huo .

( b ) Je , ni nini dhamira ya mtunzi wa utanzu ?

( c ) Andika maana ya maneno yaliyokolezwa wino .

( d ) Unafikiri huo ni utanzu wa aina gani katika kazi za fasihi ? Toa sababu mbili ( 2 ) .

SEHEMU C ( Alama 30 )

Jibu maswli mawili ( 2 ) katika sehemu hiii . Swala la tisa ( 9 ) ni la lazima .

9 . Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma , eleza namna waandishi wa diwani hizo walivyotumia kipengele cha taswira katika kazi zao , toa hoja tatu ( 3 ) toka katika kila diwani kuonesha namna ziliivyosaidia kutoa elimu kwa jamii ya kitanzania .

10 . " Waandishi wa kazi za fasihi wamebobea sana katika kuteua wahusika ambao hubeba ujumbe halisi kwa jamii ya Tanzania ." Fafanua ukweli wa kauli hii kwa kutumia wahusika watatu kutoka katika kila riwaya mbili ulizosoma .

11. " Watanzania wangefaidika na tamthiliya kama wangeishi kwa kufuata utamaduni wa kitamthiliya ." Jadili kauli hii kwa kutoa hoja tatu ( 3 ) kutoka katika kila tamthiliya kati tamthiliya mbili ulizosoma .

Shulelibrary.com